

KUMBUKA:

- Kifua kikuu sio ugonjwa wa kulogwa wala kurithi
- Mshauri mtu mwenye dalili za kifua kikuu kuwahi kwenye kituo cha huduma za afya kwa uchunguzi
- Kifua kikuu kinatibika na kuona kabisa hata kama una maambukizi ya VVU.
- Mgonjwa anapaswa kupata matibabu ya kifua kikuu mapema ili kuzuia maambukizi kwa watu wengine
- Mgonjwa wa kifua kikuu ambaye ameanza tiba siyo rahisi kuambukiza mtu mwingine, hivyo hakuna sababu ya kumtenga
- Matibabu ya kifua kikuu yanatolewa bila malipo katika vituo vya tiba vya serikali na binafsi nchini kote.



Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wazee na Watoto



Kwa maelezo zaidi wasiliana na
mtoa huduma wa / za Afya aliye karibu nawe.

Kimetolewa na:

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,
Wazee na Watoto

kupitia

Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua
Kikuu na Ukoma

S.L.P. 9083, Dar es Salaam, Tanzania.

Barua pepe: info@moh.go.tz,

Tovuti: www.ntlp.go.tz,

Toleo la 2016

FAHAMU UKWELI KUHUSU UGONJWA WA KIFUA KIKUU (TB)



TUUNGANE KUTOKOMEZA KIFUA KIKUU

UTANGULIZI

Kifua kikuu ni ugonjwa unaoathiri mamilioni ya watu kila mwaka. Yafuatayo ni maelezo muhimu ambayo kila mmoja anapaswa kufahamu kuhusu ugonjwa huu. Nchini Tanzania, takwimu zinaonyesha kuwa wastani wa watu 64,000 huugua kifua kikuu kila mwaka, sawa na wastani wa wagonjwa 176 kila siku.

KIFUA KIKUU NI NINI?

Kifua kikuu ni ugonjwa unaosababishwa na vimelea aina ya bacteria visivyoonekana kwa macho bali kwa kutumia hadubini.

DALILI ZA KIFUA KIKUU

- Kukohoa
- Homa za mara kwa mara
- Kutokwa jasho jingi kuliko kawaida hasa usiku
- Kupungua uzito na kukonda
- Makohozi yaliyochanganyika na damu

UCHUNGUZI WA KIFUA KIKUU

Njia kuu ya kugundua kifua kikuu ni kupima makohozi.

WATU WALIO KATIKA HATARI ZAIDI YA KUAMBUKIZWA KIFUA KIKUU

- Watu wanaoishi na VVU
- Watu walio katika msongamano
- Wazee zaidi ya miaka 65
- Watoto chini ya miaka mitano
- Watu wenye magonjwa ya muda mrefu - kama vile kisukari, saratani n.k
- Watu wenye lishe duni mfano - wenye utapiamlo.
- Walevi wa kupindukia

TIBA

- Matibabu ya kifua kikuu ni miezi sita
- Mgonjwa anatakiwa kunywa dawa kila siku bila kukosa
- Ni muhimu kumaliza dozi au matibabu kama ilivyoelekezwa na mhudumu wa afya
- Kumbuka, kuacha kunywa dawa za kifua kikuu kikamilifu kunaweza kusababisha vimelea kuwa sugu na hivyo kuambukiza watu wengine
- Tiba ya kifua kikuu inapatikana **bila malipo yoyote** katika vituo vya huduma za afya vya serikali na binafsi
- Matibabu yanatolewa kila siku chini ya usimamizi
- Mgonjwa anaweza kusimamiwa na

mhudumu wa afya katika kituo cha tiba au mtu aliyemchagua mwenyewe nyumbani.

JINSI YA KUZUIA MAAMBUKIZI YA KIFUA KIKUU

- Kugundua wagonjwa wote wenye dalili za kifua kikuu mapema na kuwatibu kikamilifu
- Kuepuka misongamano
- Kutotema mate au makohozi ovyo
- Kuishi kwenye mazingira safi na kuhakikisha nyumba zetu zinakuwa na mzunguko wa hewa pamoja na mwanga wa kutosha.
- Kuchanja dawa ya kinga ya kifua kikuu (B.C.G) kwa kila mtoto mchanga. Hakikisha hata kama mtoto anazaliwa nyumbani apelekwe kituo cha tiba kwa ajili ya chanjo
- Kula chakula bora

